



EMBU UNIVERSITY COLLEGE

(A Constituent College of the University of Nairobi)

2014/2015 ACADEMIC YEAR

FIRST SEMESTER EXAMINATIONS

**FIRST YEAR EXAMINATION FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION
(ARTS)**

TKS 103: HISTORICAL DEVELOPMENT OF KISWAHILI

TAREHE: NOVEMBER 30, 2015

MUDA: 14:00-16:00

MAAGIZO:

Jibu swali la **KWANZA** na maswali mengine **MAWILI**.

SWALI LA KWANZA:

- a) Onyesha umuhimu wa kusoma historia ya lugha ya Kiswahili. (Alama 5)
- b) Lugha ya Kiswahili yafaa kusanifishwa upya . Dhihirisha kauli hii kwa hoja tano. (Alama 5)
- c) Fafanua hoja tano zinazodai Kiswahili ni lugha ya Kiarabu. (Alama 5)
- d) Eleza mafanikio matano ya K.K.A.M. (Alama 5)
- e) Jadili mambo yaliyochangia usanifishaji wa lugha ya Kiswahili. (Alama 5)
- f) Fafanua jinsi Wajerumani walivyochangia kueneza Kiswahili nchini Ujerumani kabla ya uhuru. (Alama 5)

SWALI LA PILI:

- a) Fafanua dhana ya lahaja huku ukionyesha aina mbalimbali za lahaja. (Alama 10)
- b) Jadili lahaja zozote tano za Kiswahili. (Alama 10)

SWALI LA TATU:

Jadili mchango wa vyombo vifuatavyo katika maenezi ya Kiswahili Afrika Mashariki enzi ya ukoloni.

- | | |
|--------------|-----------|
| i) utawala | (Alama 5) |
| ii) dini | (Alama 5) |
| iii) vita | (Alama 5) |
| iv) biashara | (Alama 5) |

SWALI LA NNE:

Usanifishaji wa Kiswahili (1930) ni hatua muhimu katika ukuzaji na maendeleo ya lugha ya Kiswahili barani Afrika :

- | | |
|--|------------|
| a) Jadili hatua nne katika usanifishaji lugha. | (Alama 10) |
| b) Taja malengo matano na changamoto tano kuhusiana na usanifishaji wa lugha ya Kiswahili. | (Alama 10) |

SWALI LA TANO:

Lugha ya Kiswahili imewahi kuainishwa kwa kutumia mitazamo na nadharia mbalimbali. Zieleze nadharia zifuatazo katika uainishaji wa lugha ya Kiswahili.

- | | |
|----------------------------------|------------|
| a) Kiswahili ni lugha chotara | (Alama 8) |
| b) Kiswahili ni lugha ya Kibantu | (Alama 12) |

--MWISHO--